NBAA/PMO.1/1 28 Juni 2017

TAARIFA KWA UMMA

MATOKEO YA MITIHANI YA NBAA ILIYOFANYIKA MEI 2017

1.0 Utangulizi

Katika kikao cha kawaida cha 172 cha Wakurugenzi wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu kilichokaa leo Jumatano tarehe 28 Juni 2017 kimeidhinisha matokeo kwa watahiniwa waliofanya mitihani ya Bodi iliyofanyika tarehe kuanzia 2 hadi 5 Mei 2017. Mitihani hiyo ilifanyika katika vituo kumi na moja vya mitihani vilivyopo Tanzania Bara na Visiwani. Mitihani hiyo ilihusisha watahiniwa katika hatua ya Kwanza na ya Pili katika Ngazi ya Cheti cha Utunzaji wa Hesabu (ATEC I, ATEC II) zenye masomo manne kila moja na Ngazi ya Taaluma; Hatua ya Msingi (Foundation Level) yenye masomo matano, Hatua ya Kati (Intermediate Level) yenye masomo sita na Hatua ya Mwisho (Final Level) yenye masomo manne. Mitihani hii ni ya sita chini ya mfumo mpya wa elimu na mafunzo unaozingatia weledi.

2.0 Matokeo ya mitihani

2.1 Matokeo ya Jumla

Watainiwa waliosajiliwa walikuwa **7,135** kati ya hao watahiniwa **521** sawa na asilimia **7.3** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watainiwa waliofanya mitihani walikuwa **6,614** sawa na asilimia **92.7**. Kati ya watahiniwa waliofanya mitihani hiyo watahiniwa **301** ambao ni asilimia **4.6** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **190** sawa na asilimia **2.9** wamefaulu kwa kufaulu masomo walioyokuwa wameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **739** sawa na asilimia **11.2** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **1,230** sawa na asilimia **18.6** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa wengine **2,599** sawa na asilimia **39.3** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi mbalimbali na watahiniwa **2,785** waliobakia sawa na asilimia **42.1** hawakufaulu mitihani yao.

2.2 Watahiniwa waliofaulu kutunukiwa Cheti cha Utunzaji wa Hesabu (ATEC) na Shahada ya Juu ya Uhasibu (CPA)

2.2.1 Cheti cha Utunzaji wa Hesabu (ATEC)

Jumla ya watahiniwa **65** wamefaulu mtihani wa Ngazi ya Cheti (Accounting Technician Level II). Idadi hii inafanya jumla ya watahiniwa waliofaulu mitihani ya Cheti kufikia **3,761** tangu mitihani hii ianze – mwaka 1991. Kati ya watahiniwa hao wanawake ni **21** sawa na asilimia **32.3** na wanaume ni **44** sawa na asilimia **67.7**

2.2.2 Shahada ya Juu ya Uhasibu (CPA)

Jumla ya watahiniwa **410** wamefaulu mtihani wa Shahada ya Juu ya Uhasibu nchini - CPA (T). Idadi hii inafanya jumla ya watahiniwa waliofaulu mitihani ya CPA kufikia **8,007** tangu mitihani hii ianze – mwaka 1975. Kati ya watahiniwa hao wanawake ni **147** sawa na asilimia **35.9** na wanaume ni **263** sawa na asilimia **64.1**

2.3 Matokeo katika Ngazi Mbalimbali

2.3.1 Ngazi ya Cheti (Accounting Technician)

2.3.1.1 Hatua ya Awali ya Cheti (Accounting Technician Level I)

Katika ngazi ya awali ya mitihani ya Uandishi na Utunzaji wa Hesabu (ATEC I) watainiwa waliosajiliwa walikuwa **108** kati ya hao watahiniwa **05** sawa na asilimia **4.6** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watainiwa waliofanya mitihani walikuwa **103** sawa na asilimia **95.4**. Kati ya watahiniwa **103** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **14** ambao ni asilimia **13.6** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, mwingine **01** sawa na asilimia **1.0** amefaulu kwa kufaulu masomo aliyokuwa ameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **17** sawa na asilimia **16.5** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **33** sawa na asilimia **31.1** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **47** sawa na asilimia **45.6** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **24** waliobakia sawa na asilimia **23.3** hawakufaulu mitihani yao.

2.3.1.2 Hatua ya Pili ya Cheti (Accounting Technician Level II)

Katika ngazi ya uandishi na Utunzaji wa Hesabu (ATEC II) waliosajiliwa walikuwa **194** kati ya hao watahiniwa **09** sawa na asilimia **4.6** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani katika ngazi hii walikuwa **185** sawa na asilimia **95.4**. Kati ya watahiniwa waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **29** ambao ni asilimia **15.7** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja na wengine **38** sawa na asilimia **20.5** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **67** sawa na asilimia **36.2** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **73** sawa na asilimia **39.5** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **45** waliobakia sawa na asilimia **24.3** hawakufaulu mitihani yao.

2.3.2 Ngazi ya Taaluma (Professional Stage)

2.3.2.1 Hatua ya Awali (Foundation Level)

Katika Hatua ya Awali; waliosajiliwa walikuwa **607** kati ya hao watahiniwa **50** sawa na asilimia **8.2** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **557** sawa na asilimia **91.8**. Kati ya watahiniwa waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **139** ambao ni asilimia **25.0** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **02** sawa na asilimia **0.4** wamefaulu kwa kufaulu masomo waliyokuwa wameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **65** sawa na asilimia **11.7** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **206** sawa na asilimia **37.0** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **251** sawa na asilimia **45.1** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **100** waliobakia sawa na asilimia **18.0** hawakufaulu mitihani yao.

2.3.2.2 Hatua ya Kati (Intermediate Level)

Katika Hatua ya Kati; waliojisaliwa walikuwa **3,813** kati ya hao watahiniwa **336** sawa na asilimia **8.8** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **3,477** sawa na asilimia **91.2**. Kati ya watahiniwa hao, watahiniwa **44** ambao ni asilimia **1.3** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **175** sawa na asilimia **5.0** wamefaulu kwa kufaulu masomo waliyokuwa wameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **317** sawa na asilimia **9.1** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **536** sawa na asilimia **15.4** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **1,437** sawa na asilimia **41.3** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **1,504** waliobakia sawa na asilimia **43.3** hawakufaulu mitihani yao.

2.3.2.3 Hatua ya Mwisho (Final Level)

Katika Hatua ya Mwisho; waliosajiliwa walikuwa **2,413** kati ya hao watahiniwa **121** sawa na asilimia **5.0** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **2,292** sawa na asilimia **95.0**. Kati ya watahiniwa hao, watahiniwa **75** ambao ni asilimia **3.3** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **12** sawa na asilimia **0.5** wamefaulu kwa kufaulu masomo waliyokuwa wameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **302** sawa na asilimia **13.2** wamefaulu

mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **389** sawa na asilimia **17.0** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **791** sawa na asilimia **34.5** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **1,112** waliobakia sawa na asilimia **48.5** hawakufaulu mitihani yao.

4.0 Watahiniwa waliobakiza muhula mmoja kutakiwa kumaliza mitihani yao katika ngazi husika

Wapo watahiniwa 500 ambao walifaulu baadhi ya masomo katika muhula wa Mei 2015. Watahiniwa hawa wanatakiwa wawe wamefaulu masomo yaliyobakia katika ngazi husika hadi Novemba 2017. Hivyo wamebakiza muhula mmoja tu ili kufaulu masomo yaliyobakia la sivyo masomo waliyofaulu huko nyuma yatafutwa na kutakiwa kuanza upya ngazi husika.

5.0 Watahiniwa waliofutiwa masomo waliyokuwa wamefaulu

Wapo watahiniwa 420 ambao walifaulu baadhi ya masomo kuanzia muhula wa Novemba 2014. Watahiniwa hawa walitakiwa wawe wamefaulu masomo yaliyokuwa yamebakia katika ngazi husika kabla au katika muhula wa mitihani ya Mei 2017. Wanafunzi hawa walishindwa kufanya hivyo na hivyo masomo waliyofaulu yamefutwa na wanatakiwa kujisajili upya kwa ajili ya mitihani hiyo. Hii inajumuisha hata wale ambao hawakufanya mitihani katika muhula huu lakini walikuwa wamefaulu baadhi ya masomo kuanzia Novemba 2014 lakini hadi sasa hawajafaulu masomo yaliyobakia.

6.0 Pongezi

Bodi inawapongeza wale wote waliofuzu mitihani yao na kuwataka wale ambao hawajafuzu kutokata tamaa bali waongeze bidii zaidi katika masomo yao ili waweze kufanya vizuri katika mitihani ijayo ya Bodi. Bodi inawashauri kutumia vema vitabu vilivyotayarishwa na Bodi katika kijiandaa kwa mitihani yao. Pia wanashauriwa kusoma vitabu vingine vya ziada ili kuongeza ufahamu zaidi katika masomo hayo.

7.0 Mitihani inayofuata

- Mitihani ya katikati ya muhula kwa ajili ya somo la Sheria (A5 Business Laws), na masomo ya kodi (B4 Public Finance & Taxation I and C4 Public Finance &

Taxation II) itafanyika tarehe **Jumanne tarehe 29 na Jumatano tarehe 30 mwezi wa Agosti 2017 katika kituo cha Dar Es Salaam tu.**

- Mitihani ya kawaida itafanyika kuanzia **tarehe 30 mwezi Oktoba hadi tarehe 3 mwezi Novemba 2017 katika vituo vitakavyotangazwa.**

8.0 Uwasilishaji wa picha kwa ajili ya mahafali

Mahafali ya 39 ya NBAA yatafanyika tarehe 30 mwezi Septemba 2017. Tangazo rasmi kuhusu mahafali hayo lipo kwenye tovuti ya Bodi. Wale wote waliofaulu mitihani ya ATEC II na CPA (T) pamoja na wale wa CPA (T) Equivalent wanatakiwa kuwasilisha picha zao kwa ajili ya kutengenezewa vyeti kabla ya tarehe 25 Julai 2017. Tangazo ya namna ya kuwasilisha picha hizo liko kwenye tovuti ya Bodi.

Matokeo haya ya mitihani ya **85** ya Bodi yanapatikana katika tovuti ya NBAA ambayo ni www.nbaa.go.tz

CPA Pius A. Maneno
MKURUGENZI MTENDAJI